# DHIMA YA TUNGO ZA MIFANO YA MATUMIZI KATIKA KAMUSI

**James S. Mdee**

## Utangulizi

Historia ya kamusi imeonyesha kwamba haja ya kuwa na kamusi ilitokana na azma ya wazungumzaji kutaka kufahamu maana za maneno waliyoyasoma katika matini. Hii ndio sababu fasili ya kamusi ilikuwa: "Kitabu cha orodha ya maneno... pamoja na maana zake." Kamusi za kisasa hususa zile ambazo zimelengwa wanafunzi wa lugha hueleza maana za maneno pamoja na kuonyesha etimolojia, matamshi, tahajia tofauti za kidahizo, taarifa mbalimbali za kisarufi na matumizi ya kidahizo (kimaana, kimtindo na kisintaksia). Kamusi huonyesha pia mifano ya matumizi ya kidahizo katika tungo.

Umuhimu wa tungo za mifano ya matumizi haufahamiki kwa watungaji na watumiaji wa kamusi walio wengi. Kamusi nyingi hazina tungo za mifano ya matumizi ya kutosha hata kama zinadai kuwa zimekusudiwa wanafunzi wa lugha inayolengwa (Ling. TUKI 1981). Baadhi ya Kamusi huingiza tungo nyingi za mifano ya matumizi bila kutambua kuwa sio kila kidahizo katika kamusi kinahitaji mfano wa matumizi (Ling. Bakhressa 1992). Watumiaji wa kamusi walio wengi hawafahamu hazina iliyo katika kamusi wanayoitumia (Bejoint 1981), sio tu kwa sababu hawajui mbinu za kutumia kamusi ambazo zingewezesha kupembua kitomeo na kubaini taarifa mbalimbali zilizomo, bali pia kwamba hawana muda wa kuusoma kwa makini utangulizi ambapo, kwa kawaida mbinu za kuitumia kamusi huandikwa. Kutojua jinsi ya kuitumia kamusi kumechangia kwa kiasi kikubwa kutofahamika kwa dhima ya tungo za mifano ya matumizi.

Madhumuni ya makala haya ni kuonyesha nafasi ya tungo za mifano ya matumizi (vishazi na virai) katika kamusi. Katika makala haya tutaonyesha kuwa tungo za mifano ya matumizi ya kidahizo katika kamusi sio ziada isiyohitajiwa, wala kijalizo cha taarifa fulani katika kamusi, bali ni kipengele muhimu ambacho kinafafanua maana na matumizi ya kidahizo. Kwa sababu hii, ni dhahiri kuwa kutoingizwa kwa kipengele hiki katika kamusi kunaweza kuathiri utoshelevu wa vitomeo na kamusi kwa ujumla.

Katika kujadili dhima ya tungo za mifano ya matumizi tutazitalii kamusi zifuatazo za Kiswahili: *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, (TUKI, 1981) Kamusi ya Kiswahili-Kiingereza (Feeley 1991), na *Kamusi ya Maana na Matumizi* (Bakhressa 1992) na kudondoa mifano ya vitomeo inayokidhi haja ya makala haya ili kuonyesha nafasi na dhima ya mifano ya matumizi katika Kamusi. Katika mjadala huu tutazingatia mambo yafuatayo:-

1. Umuhimu wa mifano ya matumizi ya kidahizo katika kamusi.
2. Dhima kuu za mifano ya matumizi katika kamusi.
3. Uchambuzi wa tungo za mifano ya matumizi kutoka katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI 1981); *The Friendly Swahili English Dictionary* (Feeley 1991); *Kamusi ya Maana na Matumizi* (Bakhressa 1992).
4. Vidahizo visivyohitaji mifano ya matumizi.
5. Urefu wa tungo.

**Umuhimu wa mifano ya matumizi ya kidahizo katika kamusi**

Mwanafunzi wa lugha mara nyingi hupenda kujua maneno yawezayo kuchukuana na kidahizo bila kuleta mgongano wa kimantiki. Kwa mwanafunzi wa lugha, kujua jinsi ya kulitumia neno katika sentensi ni muhimu, sawa na kufahamu maana yake. Mifano ya matumizi ni muhimu katika kamusi kwani inaifanya kamusi ikamilike na ijitosheleze. Kwa hali hii ni muhimu sana katika kitomeo.

Kwa mujibu wa Landau (1984:166) mifano ya matumizi ni sehemu ya fasili ya kidahizo kwa sababu inafafanua maana ya kidahizo. Landau anaiona mifano ya matumizi kama ushahidi wa mtungaji kamusi kuhusu maelezo ya maana ya kidahizo aliyoiandika. Kwa mujibu wa Landau maelezo hayo ni maoni ya mtungaji kamusi alivyoyapata kwa kupembua miktadha mbalimbali ya neno hilo. Wasomaji wa kamusi wanaweza kuafikiana naye au kutokukubaliana naye kwa kuchambua mifano ya matumizi iliyotolewa ili kupata maana ya neno. Hii ndio sababu wanaleksikografia wanapendekeza kuwa mifano ya matumizi asili itumiwe zaidi kuliko ile ya kubuni kwani hiyo ndiyo yenye ushahidi kuwa muktadha ni wa kweli na wenye kuaminika. Aitken (1973) kama alivyonukuliwa na Drysdale (1987) katika Cowie (1987:213) naye anadai kuwa mifano ya matumizi ni muhimu zaidi kuliko fasili ya kidahizo, na ni sehemu muhimu sana ya maudhui ya kamusi. Fox (1987:136) naye anadai kuwa mifano ya matumizi ni muhimu sana katika kujifunza neno.

Umuhimu wa tungo za mifano ya matumizi unashereheshwa na Fox (1987:137) anaposema kuwa mifano ya matumizi inashadidia maana ya neno kwa kuonyesha:

(1) jinsi neno linavyotumiwa katika muktadha maridhawa,
(2) muundo wa kisarufi wa kawaida wa neno na
(3) maneno ambayo daima yanahusiana na kidahizo kitumiwapo katika lugha.

Landau (1984) akikariri hoja za Fox juu, anaongeza nyingine mbili:

(4) kuonyesha mitindo ya matumizi ya neno na
(5) kuonyesha hisia za kimatlaba.

Kutokana na fikra za Aitken, Landau na Fox tunaweza kusema kuwa tungo za mifano ya matumizi zina dhima mbili kuu:

(a) kueleza au kufafanua maana ya kidahizo na

(b) kuelekeza jinsi kidahizo kinavyotumiwa katika lugha (kufundisha lugha)

**Dhima ya kufafanua maana ya kidahizo**

Tungo za mfano wa matumizi hujaliza fasili za vidahizo ambazo maelezo yake hayajitoshelezi. Kufafanua au kueleza maana ya kidahizo katika sentensi za mfano humsaidia mtumiaji kamusi:

(i) Kutofautisha maana za kidahizo zinazokaribiana na kuzifanya bayana.

(ii) Kufafanua fasili zisizo wazi na kuzifanya dhahiri zaidi ili zieleweke.

**Dhima ya kuelekeza matumizi ya kidahizo.**

Tungo za mifano ya matumizi huonyesha ruwaza ya sintaksia ya kidahizo. Hubainisha nafasi ya kidahizo katika tungo ikionyesha maneno ambayo daima huonekana yakifungamana na kidahizo. Sentensi za mifano humsaidia mtumiaji wa kamusi:

(a) kuchagua ruwaza sahihi ya kisarufi inayosadifu neno analolitafuta ili kuibua maana iliyokusudiwa.

(b) kuchagua maneno yanayochukuana na kidahizo ambayo yanakubalika kwa wazawa wa lugha inayohusika.

(c) kutunga sentensi sahihi kwa mujibu wa kanuni za kisarufi zinazokubaliwa na wazawa wa lugha.

(d) kutambua mtindo (rasmi, sio rasmi) ambamo neno hutumiwa.

Dhima hii ni muhimu sana kwa watumiaji wa kamusi ambao ni wanafunzi wa lugha inayolengwa. Wazawa wa lugha nao pia wanahitaji mifano ya matumizi japo kwa uchache hususa kwa maneno yasiyotumika mara kwa mara na ambayo ruwaza yake haifahamiki na wengi. Tungo za mifano katika kamusi hazina budi kuakisi matumizi ya kila siku ya neno. Mifano hii sio tu kuwa ni sahihi kisarufi bali pia ni tungo ambazo zinaweza kurudiwa tena (katika maandishi au mazungumzo).

Sentensi za mifano katika kamusi nyingi ni mifano ya kubuni. Kamusi chache zina tungo zilizonukuliwa kutoka katika matini asili kama vile vitabu, magazeti au kanda za kunasa sauti ambamo hotuba zimehifadhiwa. Zgusta (1971), Landau (1984) na Sinclair (1985) wanapendekeza mifano asili itumike zaidi kuliko ya kubuni. Sababu zinazotolewa zenye kupendelea sentensi asili ni mbili.

(1) zinatoa ushahidi wa namna neno linavyotumiwa. Sentensi hizi ni kielelezo sahihi cha kuigwa cha matumizi ya neno.

(2) zinamsaidia mtumiaji kamusi kudadisi maana ya neno ambayo inatokana na muktadha ambapo neno lipo.

Tatizo la kutumia sentensi asili ni kwamba wakati mwingine zinakuwa na maneno magumu hivyo kwamba huifanya sentensi isieleweke (Landau 1984; Kirkpatrick 1985). Kwa hali hii inashauriwa kuwa pale inapowezekana kutumia sentensi asili itumike, vinginevyo tungo ya kubuni iliyosawidiwa vyema na kuthibitishwa na wazawa wa lugha itafaa pia.

Akisisitiza manufaa ya tungo za mifano, Fox (1987) anasema kuwa mifano ya matumizi humsaidia mwanafunzi wa lugha kuitambua maana anayoitafuta katika kidahizo chenye maana nyingi kwa kupembua sentensi za mifano zilizo katika kitomeo ili kupata sentensi inayofanana na ile yenye neno ambalo maana yake anaitafuta katika kamusi. Mtumiaji kamusi anapoipata sentensi hiyo ataweza kutambua maana anayoitafuta. Kutoingiza mifano ya matumizi katika kitomeo chenye mlolongo wa sinonimu humtatiza mtumiaji kamusi asitambue maana ya neno anayoitafuta kati ya maana zilizoorodheshwa.

Pamoja na umuhimu wa sentensi za mifano kwa mtumiaji wa kamusi itafaa kusisitiza kuwa sio kila kidahizo kinahitaji sentensi ya mfano wa matumizi. Vidahizo ambavyo vinastahili kupatiwa tungo za mfano wa matumizi ni vile ambavyo huchukuana na maneno maalum. Vidahizo visivyochukuana na maneno maalum havihitaji kuwa na mfano wa matumizi. Nomino nyingi, kwa mfano hazifungamani na maneno maalumu, kwa hivyo hazihitaji mifano ya matumizi. Lakini nomino zinazochukuana na vitenzi maalum kama vile '*chenga*' kama katika *piga chenga* ndizo zinastahili kupata mifano ya matumizi vivyohivyo, vivumishi vinavyochukua nomino mahsusi vipatiwe mifano ya matumizi.

Kidahizo chenye maana zaidi ya moja hakina budi kupatiwa mifano ya matumizi inayolingana na idadi ya maana ili kudhihirisha maana tofauti pamoja na nafasi ya kidahizo kati ya maneno yanayoandamana nacho na kuibua hizo maana tofauti.

Maana moja ya kidahizo yaweza pia kupatiwa mifano zaidi ya mmoja. Hii ni muhimu iwapo maana ni ya jumla na ndani yake kuna maana ndogondogo kuu moja zinazotofautiana kidogo. Tofauti hizi zinaweza kudhihirishwa kwa mfano wa matumizi. Kwa kuwa mifano ya matumizi huonyesha maneno ambayo kidahizo huambatana nayo, basi mifano hiyo inaweza kuwa ni virai, vishazi au sentensi.

Tungo funge kama vile methali, nahau na misemo hazisadifu kuwa tungo za mfano wa matumizi kwani zinaonyesha matumizi ya kipekee ya maneno. Matumizi haya hayaakisi matumizi ya kawaida ya maneno katika lugha. Aidha maana ya tungo funge ni mahsusi na haiibui maana ya kawaida ya maneno yanapotumika katika lugha ya kawaida.

**Tungo za mifano ya matumizi katika kamusi za Kiswahili**

*Kamusi ya Kiswahili* Sanifu (TUKI 1981), *Kamusi ya Kiswahili-Kiingereza* (SED) (Feeley 1991) na *Kamusi ya Maana na Matumizi* (KMM) (Bakhressa 1992) zina

tungo za mifano ya matumizi ya vidahizo vilivyomo. Baadhi ya tungo zinadhihirisha uhusiano wa kidahizo na maneno mengine katika tungo.

Mfano$_1$ Kurani *takatifu*
kwa *ajali*
weka *amana*
acha *ajizi*
(Feeley 1991)
Juma hili zima Bwana harusi *anakula fungate*
Mtoto *amefunga choo*
Amekuja hapa *kwa ajili ya* mama
(Bakhressa 1992)

Maneno yaliyo katika italiki ni vidahizo kutoka Feeley (1991) na Bakhressa (1992). Tungo hizi zinaonyesha maneno ambayo huchukuana mara kwa mara na vidahizo hivi. Kwa mfano: Kurani huambatana na takatifu (hata hivyo wazungumzaji wengi huambatanisha Kurani na *tukufu)*. Vivyohivyo, kidahizo *ajili* huchukuana na *kwa* pamoja na *ya* (*kwa ajili ya*), *ajizi* huchukuana na *acha* kama vile (*acha ajizi*) n.k.

Mifano hii inamtahadharisha mtumiaji kamusi kutambua kuwa maneno yanapokuwa katika tungo huwa na uhusiano wa kiuteuzi. Neno huteua neno fulani au maneno fulani tu, au hukubali kuteuliwa na neno au maneno fulani. Kwa mfano, neno *ajizi* hukubali kuteuliwa na *fanya* au *acha* lakini halikubali kuteuliwa na vitenzi vingine kama vile *zuia* au *tenda*.

Mfano$_2$ acha ajizi
fanya ajizi
*tenda ajizi
*zuia ajizi

Mifano 1 na 2 inaonyesha dhima ya kamusi ya kufundisha lugha, Inaonyesha nafasi ya kidahizo katika tungo ikibainisha neno au maneno yanayoambatana na kidahizo; Mfano$_3$ unadhihirisha hili.

Mfano$_3$ Amekuja hapa kwa *ajili* ya mama
Bwana harusi anakula *fungate*
Mipango yake inakwenda *tenge*
(Bakhressa 1992: 6)

**Tungo zenye kujaliza maana ya fasili**
Mbali na tungo zenye kuelekeza namna kidahizo kinavyotumika katika lugha, tungo za mfano wa matumizi zimetumika pia kueleza maana ya kidahizo. Tungo za Mfano$_4$ zinadhihirisha tofauti za maana za neno *acha:*

Mfano $_4$ Juma ametu*acha* mkono
Kuku ame*acha* watoto wake
Ali amemw*acha* mkewe
Hamisi ali*acha* mali nyingi, mke na watoto
Mtoto ameki*acha* chakula nusu sahani
(TUKI 1981: 1)

Tungo za Mfano$_4$ juu ya zinadhihirisha maana tofauti za neno *acha*. Aidha tungo za mfano wa matumizi huweza kukamilisha fasili ya kidahizo ambayo haikujitosheleza.

Mfano$_5$

**saa** *ji* 1 muda unaochukua dakika sitini, sehemu moja ya ishirini na nne inayokamilisha siku: *Safari yangu ilichukua saa tatu nzima:*

**sababisha** *kt* fanya kitu fulani kiwe au kitokee; anzisha. *Njaa ndiyo iliyomsababisha akaiba.*

**sababu** *ji* 1. kitu kinachofanya kitu kingine kitokee; chanzo, asili. *Hebu nieleze sababu ya mwalimu kukupiga.*

**salala** *ki* tamko la kuonyesha mshangao.*Salala Itakuwaje mtu mmoja anywe pipa zima la maji.* (TUKI 1981:245 ff)

Fasili ya *saa* haitoshelezi hasa kwa mtu asiyefahamu hesabu za wakati k.v. siku, saa, dakika, nukta n.k. Sentensi ya mfano inaitoa dhana ya saa kutoka kwenye dakika 60 au $^1/_{24}$ ya siku na kuiingiza katika muda fulani unaotumiwa kufanya jambo. Fasili ya *sababisha* haielezi vya kutosha maana ya kidahizo hiki. Sentensi ya mfano inaifanya fasili ikamilike na maana aya neno ieleweke vizuri zaidi. Sentensi ya mfano wa *salala* inaonyesha jambo linaliweza kumshangaza mtu.

**Vidahizo visivyohitaji mfano wa matumizi**
Maneno ambayo hayafungamani na maneno maalum hayana lazima ya kuonyeshwa mfano wa matumizi.

Mfano$_6$ **abiria** mtu anayesafiri kwa basi mashua, garimoshi, meli, jahazi, ndege, matatu, daladala n.k. *Abiria wote wameombwa kufika kwenye kituo cha basi kabla ya saa moja asubuhi*

**barabara** 1 njia pana, njia kuu *Barabara ya hapa na Nakuru ni nzuri* (Bakhressa 1992:

Vidahizo hivi havikuhitaji mifano ya matumizi. Ni muhimu kutambua kuwa sio kila kidahizo kinahitaji mfano wa matumizi.

**Tungo ya mfano wa matumizi ya kidahizo zenye dhima ya fasili.**
Baadhi ya vidahizo havina maana ya kileksimu. Vidahizo hivi havikufasiliwa, na badala yake kidahizo kimepewa tungo ya mfano wa matumizi pekee. Tungo hizi hutumiwa badala ya fasili. Tungo hizi humsaidia mtumiaji kudadisi maana ya vidahizo kutokana na muktadha wake au fasiri ya tungo iliyotolewa.

Mfano$_7$ **shake** *ji* hutumika katika msemo: *Ingiwa na shake* = lia bila kutoa sauti

**tebwere** *kl* hutumika kusisitiza kulainika kwa kitu; *Ametebwereka tebwere* = lainika sana.

**tumbua** *kt* hutumika katika msemo: ~ *macho* = toa macho.

(TUKI 1981 : 253 ff)

Japokuwa vidahizo *shake, tebwere* na *tumbua* havina fasili yenye kueleza maana yavyo, tungo za mifano zimeonyesha maana za maneno yanayoambatana na vidahizo hivyo.

**Urefu wa sentensi za mfano**
Nafasi katika kamusi ni kitu adimu na chenye thamani kubwa. Hii ndio sababu watunzi wa kamusi hutumia lugha ya msimbo kuingiza taarifa mbalimbali za kisarufi. Sentensi za mfano wa matumizi halikadhalika hazina budi kuwa fupi kadri inavyowezekana. Kama ilivyokwishaelezwa, sio kila kidahizo kinahitaji mfano wa matumizi. Jambo la kuzingatia ni umuhimu wa tungo hizo kwa kidahizo kinachohusika. Iwapo kidahizo hakiambatani na maneno mahsusi wakati wote katika lugha, basi kidahizo hicho kitahitaji fasili tu. Kwa mantiki hii nomino nyingi hazihitaji tungo za mfano.

Sentensi za mfano wa matumizi katika baadhi ya vidahizo vya Kamusi za Kiswahili ni ndefu mno.

Mfano$_8$ **amani** hali ya kuwa salama; hali ya kutokuwa na ghasia au fujo: *Wafanyakazi walifanya maandamano ya amani walipokuwa wanadai wapewe nyongeza ya mishahara.*

**Alhamisi** siku inayofuata Jumatano. *Siku ya Alhamisi si siku ya mapumziko, ni siku ya kawaida ya kufanya kazi.*

**Kichocho** ugonjwa wa kukojoa damu. *Wagonjwa wenye kichocho hufanyiwa uchunguzi ili kuthibitisha kuwa hawana viini vya ukimwi kwenye damu yao.*
Bakhressa (1992: 9 ff)

Sentensi za mfano kwa vidahizo hivi ni ndefu. Isitoshe maneno hayo hayaambatani na maneno yoyote mahsusi. Ili kutumia nafasi kidogo, inafaa mfano wa matumizi uwe ni sentensi sahili au kishazi kimoja badala ya sentensi changamano au ambatano. Kilicho muhimu katika tungo ni kuonyesha nafasi ya kidahizo katika tungo na uhusiano wake na maneno mengine katika tungo. Sentensi za Mfano$_8$ sio sentensi sahili wala kishazi kimoja. Sentensi ya mfano ya kidahizo *amani* ni sentensi changamano.

(a) Wafanyakazi walifanya maandamano ya *amani*
(b) (Wafanyakazi) walipokuwa wanadai wapewe nyongeza ya mishahara.

Kishazi (b) hakionyeshi matumizi ya kidahizo *amani*. Kwa hali hii hakikuwa muhimu katika kidahizo hicho. Kishazi (a) kina kidahizo *amani*. Tungo hii inaonyesha kuwa amani inahusiana na maandamano, kwani ndiyo yanakaribiana na kuunganishwa na kiunganishi 'ya': *maandamano ya amani*. Kidahizo hiki kinahusiana na maneno mengine pia kwa muundo huuhuu. Kwa mfano: mtaa wa amani, mji wa amani, nchi ya amani, taifa la amani[1].

Hii inaonyesha kuwa neno amani halina uhusiano maalum na maandamano. Kwa hivyo halikustahili kuwa na huu mfano wa matumizi.

Kidahizo *kichocho* kina mfano wa matumizi ambao ni sentensi ambatano:

(a) Wagonjwa wenye *kichocho* hufanyiwa uchunguzi
(b) Uchunguzi wa kuthibitisha kuwa (wagonjwa) hawana viini vya ukimwi kwenye damu zao.

Kishazi (b) hakina kidahizo *kichocho* na wala hakionyeshi matumizi ya kidahizo hiki. Kwa hivyo hakina umuhimu kwa kidahizo *kichocho*. Kishazi (a) ndicho chenye mfano wa matumizi wa *kichocho*. Neno hili linaambatana na "-enye" (wenye kichocho) na kitenzi "fanyia" (kichocho hufanyiwa). Katika makundi haya mawili neno kichocho linahusiana zaidi na -enye na kuunda kivumishi

---

[1] Bakhressa 1992:9 ameorodhesha makundi haya ı maneno yenye kuambatana na neno amani.

kinachovumisha wagonjwa (wenye kichocho). Neno -enye sio pekee linalounda kivumishi likiambatana na kichocho. Kichocho huweza kuchukuana pia na -a ya uhusiano na kudhihirisha dhima ya kuvumisha: **ugonjwa wa kichocho**, **dawa ya kichocho, vijidudu vya kichocho** n.k. Isitoshe nomino nyingi huambatana na -enye au -a, na kuunda kivumishi. kwa mfano: **wadi ya wagonjwa; wagonjwa wenye ukimwi**. Kwa hali hii, **-enye** sio kiambatano mahsusi au cha lazima kwa neno kichocho.

Sentensi za mfano wa matumizi za **Mfano**$_8$ juu sio tu kuwa ni ndefu mno bali pia hazina umuhimu wowote kwa vidahizo vinavyohusika kwa sababu hazionyeshi dhima ya kueleza maana ya kidahizo wala dhima ya kuelekeza matumizi ya neno katika lugha.

Mifano ya sentensi fupi ni kama zile zilizomo katika TUKI 1981 kama **Mfano**$_9$ chini unavyoonyesha.

Mfano$_9$

**sembuse** *kl* tamko linalotumika katika kulinganisha baina ya vitu (ili) kuonyesha tofauti iliyoko: *Kaka yako alishindwa sembuse wewe!*

**shabihi** *kt* fanana na: Amemshabihi sana ndugu yangu

**shikiza** *kt* fanya jambo kwa muda wakati unasubiri kupata kilichobora zaidi: *Gari hili ni bovu lakini najishikiza nalo*. (TUKI 1981: 251)

Tungo zote hizi ni sentensi sahili zenye kidahizo kinachohusika. Sentensi yenye kidahizo **sembuse** inaonyesha kuwa neno hili hutokea baada ya kitenzi na kufuatwa na nomino au kiwakilishi nafsi ambacho hulinganishwa na nafsi ya mtajwa (mtenda au mtendwa) katika tungo.

Feeley (1991) ana tungo fupi ambazo aghalabu ni kirai (kundi tenzi au kundi nonimo).

Mfano$_{10}$

**acha** stop, quit, give up; leave behind
*acha kazi*, resign
*acha kwenye mataa,* fail to show up
*acha aseme*, let him/her speak

**achisha** get rid of, force to go
*achisha kazi*, fire sb/force to go
*achisha ziwa*, wean a baby

**andika** write: arrange, prepare
*andika barua*: write a letter
*andika meza*: set the table

**ajali** an accident, fate
*kwa ajali*: accidentally

**ajili** cause, sake
*kwa ajili ya*: because of, for the sake of
(Feeley 1991: 1 ff)

Tungo hizi zinaonyesha maneno ambayo huambatana mara kwa mara na kidahizo. Viambatano hivi vina muundo wa kinahau kwa mfano *acha kazi*, *achisha ziwa*, *andika meza* n.k. Tungo nyingine zinaonyesha uhusika wa vitenzi k.m. *andika barua*.

**Hitimisho**

Makala haya yameonyesha kuwa mifano ya matumizi haionyeshi tu jinsi kidahizo kinavyotumiwa katika lugha, bali hudokeza pia maana ya kidahizo. Kwa mintaarafu hii mifano ya matumizi ni sehemu muhimu katika kitomeo cha kamusi. Kutoingizwa katika kamusi kunaweza kuathiri uwezo wa kamusi wa kumsaidia mtumiaji kamusi kuisimba au kuisimbua lugha. Makala haya yameonyesha pia kuwa mfano wa matumizi unaweza kutumiwa badala ya fasili ya neno na kudokeza maana ya neno kutokana na muktadha kidahizo kinachohusika kilipotumika.

Katika kuhitimisha makala haya itafaa kusisitiza tuliyokwishaeleza mwanzo wa makala haya kuwa dhima ya tungo za mifano ya matumizi katika kamusi haifahamiki kwa watunga kamusi na watumiaji kamusi. Tunatumaini kuwa makala haya yamesaidia kutoa mwanga japo kidogo. Tunatarajia kuwa tumefaulu kuwachochea wanafunzi wa lugha kudadisi tungo za mifano ili kupata ufafanuzi, wa kutosha wa kisemantiki na kisintaksi wa vidahizo katika kamusi wanazozirejelea. Kwa watungaji kamusi, mjadala huu utakuwa changamoto kwao. Je mifano ya matumizi katika kamusi zao unazingatia misingi ya leksikografia mintaarafu kipengele hiki muhimu cha kamusi?

## MAREJEO


Bakhressa, S.K.(1992)*Kamusi ya Maana ya Matumizi*. Nairobi: Oxford University Press.

Bejoint, H. (1981) "The Foreign Student's Use of Monolingual Dictionaries: A study of Language Needs and Reference Skills". Katika *Applied Linguistics* Vol. II no 3 kur. 207 - 222.

Cowie, A (mhariri) (1987) *The Dictionary and the Language Learner* Tuebingen: Max Niemeyer Verlag.

Drysdale P.D.(1987) The role of examples of a learner's dictionary. Katika Cowie (mhariri) *The Dictionary and the Language Learner.*

Feeley G. (1991) The *Friendly Swahili-English Dictionary*. Denmark: MSC

Fox G. (1987) The case for examples. Katika Sinclair J.M.(mhariri) *Looking up*

Ilson, R (mhariri) (1985) *Dictionaries, Lexicography and Language.* Oxford: Pergamon Press na The British Council.

Kirkpatrick B. (1985) A Lexicographical Dialemma: Monolingual Dictionaries for the Native Speaker and the Learner. Katika Ilson R. (mhariri) *Dictionary, Lexicography and Language Learning.*

Landau S. (1984) *Dictionaries. The Art and Craft of Lexicography.* New York: The Scribner Press.

Lemmens, M. & Wekker, H. (1986) *Grammar in English Learner's Dictionaries.* Tuebingen: Max Niemeyer Verlag.

Sinclair, J.M. (1985) LexicographicEvidence. Katika Ilson R. (mhariri) *Dictionaries, Lexicography and Language learning.*

Sinclair, J.M. (mhariri) (1987) *Looking up.* London na Glasgow:Collin ELT

TUKI (1981) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam: Oxford University Press.

Zugsta L. (1971) *Manual of Lexicography.* The Hague: Academia Prague, Mouton.